

**Nganyeni primay school – Mgeni Rasmi speech Friday 26th
September 2003**

Asanteni sana kwa kunikaribisha leo kuwa Mgeni Rasmi wenu wa mahafali ya darasa la saba mwaka huu.

Nimefurahi kuja hapa shuleni na nimepewa heshima ya kuwa Mgeni Rasmi.

Nimefurahi jinsi nilivyoona na nilivyosikia kuhusu shule hii yenu ya Nganyeni.

Hasa nimefurahi kusikia kwamba walimu wanajitolea kufundisha Jumamosi na Jumapili – na matokeo yapo kwa sababu kutoka mwaka tisini na tisa, mlivyotaja, wanafunzi wengi wamefaulu mitihani ya darasa la saba.

Wanafunzi wa darasa la saba mwaka huu, nyinyi mmemaliza sasa kusoma hapa. Baadhi yenu mtakuwa na nafasi ya pekee kusoma shule ya sekondari. Mkisoma sekondari kweli mna nafasi nzuri maisha yenu. Wengine mtakwenda kusoma shule ya ufundi, na pia mna nafasi kujenga ujuzi na utaalumu na kuweza kuajiriwa au kujiajiri.

Lakini leo nafikiri hamna uhakika mtafanya nini kwa sababu bado hamjapata matokeo ya mitihani. Lakini bila shaka wengi, labda zaidi ya nusu, yenu mtabaki nyumbani bila kwenda kusoma popote.

Nataka kuchukua nafasi kujaribu kusaidia nyinyi mtakaobaki nyumbani.

Cha kwanza ni kuendelea na matumaini, na kuwa na utaratibu. Kila asubuhi mnapaswa kuamka na lengo la siku – kufanya kitu, bila kukaa hovy hovy.

Ukiweza kulima utaweza kupata pesa na kuanza kujenga maishi yako. Ukiweza kupata ardhi kidogo – hata mita tano kwa tatu kwa mfano – ukiohesha mboga za majani, na ukimwagilia kila siku na ukipalilia – baada ya wiki au mwezi utakuwa tayari kuuza mboga zako. Kazana tu, na utapata faida.

Si vibaya kujitolea – siku ya wananchi kujenga taifa – kama huna kazi nyingine – nenda tu. Watu wakifahamu una hamu ya kufanya kazi na kwamba unafanya kazi kwa bidii – utatambuliwa an utajulikana. Halafu

unaweza kupewa kazi ya kulipwa. Ukijificha nyumbani bila malengo nani atakufahamu kuweza kukusaidia?

Kwa hiyo naomba kila mmoja kutokusahau nidhamu ya shule – ya kuamka mapema asubuhu na kufanya kazi mpaka masaa ya mchana. Endelea pia kusoma – tafuta magazeti na vitabu, na pia sikiliza redio kufahamu habari za dunia.

Msikate tamaa mkikosa nafasi kwenda kusoma sekondari au shule ya ufundi, bado unaweza kujenga maisha mazuri, lakini itabidi wewe kufanya kazi na kuwa na lengo la kujenga jina lako kwa wote kutambua wewe ni mzuri, na ni mshindi, na pia ni mwaminifu.

Nawatakieni kila la heri.

Basi sasa, nyinyi mnaobaki shuleni – walimu na wanafunzi. Nimesikitika kusikia kuhusu matatizo ya ofisi ya walimu, choo cha walimu na hali ya majengo kwa ujumla.

Sitaweza kusaidia chochote mapema, kwa sababu tuna utaratibu na mipango kwa mwaka huu na ujao. Lakini nimeshapokea maombi na nitajitahidi kusaidia na kuondoa shida ya _____

Lakini sio kesho, inaweza kuchukua muda kidogo.

Nimeshasema vya kutosha. Asenteni tena kwa kunikaribisha hapa leo.